



Nilisikia upopo.

Ulivuma na kupita
kwa kasi karibu na
makao yetu.



Upepo huo
ulikuwa mkali.

Uliibandua tiara
yangu kutoka
mkononi.



Niliifuata tiara
yangu.

Lakini, upepo huo
mkali ulinisukuma
mbali nayo.



Upepo huo uligeuka
na kuwa dhoruba.

Dhoruba hiyo
iliienua tiara yangu
juu zaidi.



Dhoruba hiyo ya
kutisha, ilinimeza
mzima mzima!

Sikuweza kuona
chochote wala
kugusa chochote.



Niliikumbuka tiara
yangu nzuri.

Ilikuwa wapi?

Labda ilikuwa
imenaswa mtini.



Au labda, ilikuwa
bado inapeperuka
hewani.



Mwishowe, dhoruba
hiyo kali ilipunguka.

Mimi nilikuwa bado
ninazunguka.




Nilipotulia,
nilitazama mahali
nilipokuwa.

Nilijiuliza, "Upepo
ule mkali umeanda
wapi?"



Sikuionia tiara yangu
nzuri popote.

Sikuusikia tena
upepo ukivuma.



Labda siku iliyofuata,
ningeipata tiara
yangu nzuri.



La muhimu kwangu
ilikuwa kwenda
zangu nyumbani,
mbali na upemo
hatari.